

Abstract

Tasnifu hii inahusu uhalisia na uhalisiajabu katika riwaya za Said Ahmed Mohammed (*Babu Alipofufuka*) na Tom Olali (*Watu wa Gehenna*). Katika utafiti huu tumechunguza uhalisiajabu katika kiwango cha wahusika na mandhari katika riwaya hizi teule tukiongozwa na nadharia ya uhalisiajabu. Ili kufikia malengo yetu, utafiti huu umegawanywa katika sura tano. Katika sura ya kwanza, tumetanguliza mada yetu, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, msingi wa nadharia, yalioyoandikwa kuhusu mada yetu, na njia za utafiti. Katika sura ya pili, tumechunguza hatua za mwanzo za uhalisiajabu ambazo ni uhalisia hakiki, uhalisia wa kijamaa hadi kufikia uhalisiajabu. Tumetambua ya kwamba waandishi waliotumia uhalisia kama vile Said A. Mohammed na K.W. Wamitila wamegeukia mtindo wa uhalisiajabu ili waweze kuyazungumzia mambo ambayo hawangeweza kuweka wazi kwa mtindo wa uhalisia. Katika sura ya tatu, tumechunguza na kubainisha vipengele vya uhalisiajabu katika viwango vya wahusika na mandhari yenye matukio ya uhalisia na uhalisiajabu katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*. Katika sura ya nne, tumebainisha wahusika na mandhari yenye matukio ya uhalisia na uhalisiajabu katika riwaya ya *Watu wa Gehenna*. Katika sura ya tano, tumetathmini matokeo ya uchunguzi wetu kwa kurejelea madhumuni na nadharia tete zetu. Tumetoa hitimisho na mapendekezo ya utafiti wa baadaye.